# Je Uko Tayari?

## (Are You Ready?)

Na

Ellis P. Forsman

# Je Uko Tayari?

## (Are You Ready?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 10, 2011

# Je Uko Tayari?

## Luka 22:31-34

Biblia ina sisitiza maneno kwa kuzitumia kila mara.

Mfano: Maneno kama “saba”, “sabini”, “ hekima”, na “upendo”.

Neno mhimu katika somo hili ni – “Tayari”

Tutajifunza njia tofauti ambazo neno hili hutumiwa.

## Petro alisema, “Bwana, Niko tayari kwenda na wewe.”

Luka 22:31-34, “*Akasema, Simoni, Simoni, tazama Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike, nawwe utakapoongoka waimarishe ndugu zako. Akamwambia, Bwana niwapo pamoja nawe mimi ni tayari kwenda gerezani au hata kifoni. Akasema, nakuambia Petro, jogoo hatawika leo, kabla wewe hujanikana mara tatu ya kuwa hunijui.*”

Wakati fulani, kwa matendo yetu watu wanaweza kufikiri kwamba tuko tayari, kama jinsi Petro alivyodhani yuko tayari.

Watu wengi katika ulimwengu wa dini wanadhani kwamba wako tayari.

Mat. 7:21-23, “*Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*”

Yesu alitangaza kukanwa. Petro alisema alikuwa tayari, lakini hakuwa tayari.

Baadaye alimkana Bwana. Luka. 22:54-62, “*Wakamkamata, wakamchukua wakaenda naye nyumbani kwa kuhani mkuu. Na Petro alimfuata kwa mbali. Na walipokwisha washa moto katikati ya kiwanja, waliketi pamoja naye Petro akaketi kati yao. Ndipo mjakazi mmoja akamwona ameketi mwangani, akamkazia macho akasema na huyu alikuwa pamoja naye. Akakana akisema, Ee mwanamke simjui. Baadaye kitambo kidogo mtu mwingine alimwona akasema, wewe nawe u mmoja wao. Petro akasema Ee mtu si mimi. Halafu yapata saa moja mtu mwingine alikaza kusema, Hakika na huyu alikuwa pamoja naye, kwa*

*kuwa yeye pia ni Mgalilaya. Petro, akasema ee mtu sijui usemalo. Na papo hapo alipokuwa katika kusema, jogoo aliwika. Bwana akageuka akamtazama Petro. Petro akalikumbuka lile neno la Bwana jinsi alivyomwambia, leo kabla hajawika jogoo utanikana mara tatu. Akatoka nje akalia kwa majonzi.*"

Tunaambiwa kufuata nyayo za Yesu. 1 Pet. 2:21, "*Kwa sababu ndiyo mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake.*"

Na kwamba tujikane wenyewe. Mat. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate.*"

Mfano: Kijana tajiri angelipa gharama. Luka 18:18-24, "*Tena, mtu mkubwa mmoja alimwuliza akisema, Mwalimu mwema, nifanye nini ili niweze kuurithi uzima wa milele? Yesu akamwambia, mbona unaniita mwema? Hakuna aliyemwema ila mmoja, naye ndiye Mungu. Wazijua amri; usizini, usiue, usiibe, usishuhudie uongo. Waheshimu baba yako na mama yako. Akasema hayo yote nimeyashika tangu utoto wangu. Yesu aliposikia hayo alimwambia, umepungukiwa na neno moja bado; viuze ulivyonavyo vyote, ukawagawanyie maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. Lakini aliposikia hayo alihuzunika sana, maana alikuwa na mali nyingi. Yesu alipoona vile alisema, kwa shida gani wenye mali watauingia ufalme wa Mungu!*"

## Kuwa tayari siku zote kutoa jibu

1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu lakini kwa upole na kwa hofu.*"

## Kufanya hivyo ni lazima tujifunze.

2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

Je nia yetu ni kama ile ya yule kijana tajiri? Je tunataka kumtumikia Yesu, na hatuko tayari kujitoa kwa ajili Yake?

Masaa mengi yanatumika katika ulimwengu huu uliozeeka tukijianda kwa ajili ya maisha mazuri. Vipi kuhusu maisha yetu ya Ukristo?

Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

## Nia njema ni muhimu.

- 1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari ya tumaini lililo ndani yenu, lakini kwa upole na hofu.*"
- Kol. 4:6, "*Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu.*"
- 2 Tim. 2:25, "*Akiwaonya kwa upole wao washindanao naye ili kama ikiwezekana Mungu awape kutubu na kuijua kweli;*"

## Paulo alisema, "Niko tayari kuihubiri injili."

Rum. 1:15, "*Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnao kaa Rumi.*"

Kwa nini Paulo alitaka kuhubiri? Hakuionea haya. Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Aliamini kwamba kuhubiri injili ilikuwa ni uweza wa Mungu (angalia msitari hapo juu). Alihisi kwamba alidaiwa kitu na Wayahudi na Mataifa pia kuwahubiria. Rum. 1:14, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.*"

Hilo ni sehemu ya tatizo ambalo Wakristo wanalo leo. Hawahisi kwamba wanadaiwa na ulimwengu chochote.

Paulo alijua kwamba wasiotii watapotea, hivyo akataka kuwahubiria.

2 Thes. 1:7-8, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasio mjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu.*"

Je una upendo wa kutosha na kujali kwa jirani yako kwa kujaribu kumwokoa? Au unahisi kwamba Wakristo wanapaswa kutunza dini yao kwao wenyewe?

Haya yanapaswa kututia changamoto kuhubiri injili, pia.

## Je uko tayari katika huduma ya ibaada kwa Kristo?

Hili ni swala la nia na kujiandaa.

Yesu na mitume walikuwa na wakati uliopangwa walipokutana pamoja kwa ajili ya Pasaka.

- Luka 22:7-8, "*Ikafika siku ya mikate isiyotiwa chachu, ambayo ilipasa kuchinja pasaka. Akawatuma Petro na Yohana akisema, nendeni mkatuandalie Pasaka tupate kuila.*"
- Luka 22:13-14, "*Wakaenda wakaona kama alivyowaambia, wakaiandaa pasaka.*"

Vipi kama kituo cha redio kiwatangazie jamii kwamba kila mtu atakayeingia katika uwanja wa mpira kabla ya saa 10:00 asubuhi atapokea $500? Kutakuwa na msitari mrefu hata kabla ya matangazo kuisha pamoja na mlolongo wa magari.

Utajiri wa mbinguni ni mkuu kuliko $500?

Mat. 16:26, "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*"

## Kwamba wao (matajiri) wawe tayari kugawa

1 Tim. 6:17-18, "*Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. Watende mema wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo.*"

Kumbuka kijana tajiri. Hatuwezi kuwa Wakristo wazuri tusiposhirikiana.

Mungu alishirikiana na sisi Mwanaye. Yohana 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Tunapaswa kuonyesha ukarimu na kutokuwa wabinafsi. Luka 10:30-37, "*Yesu akajibu akasema mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi wakamvua nguo, wakamtia jeraha wakaenda zao, wakimwacha karibu na kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona akapita kando. Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo, ; na alipomwona alimhurumia, akakaribia akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akisema mtunze huyu na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe katika hao watatu ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi. Akasema ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo.*"

Kanisa la kwanza lilifanya mambo haya.

- *Wakiuza mali zao na vitu vyao walivyokuwa navyo na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.*"
- Mdo. 4:34-35, "*Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza wakavileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa. Wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji.*"
- Yak. 1: 27, "*Dini iliyo safi isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*"
- Tito 3:1, "*Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema.*"

## Paulo alisema, "***Niko tayari...kufa.***"

Mdo 21:13, "*Ndipo Paulo alipojibu mnafanya nini, kulia na kunivunja moyo? Kwa maana mimi licha ya kufungwa, ni tayari hata kuuawa katika Yerusalemu kwa ajili ya jina la Bwana Yesu.*"

Agabo na ndugu wengine walijaribu kumkataza Paulo asiende Yerusalemu. Wakashindwa. Paulo alikamatiwa Yerusalemu na baadaye akafungwa Rumi, mahali ambapo alifia ghafla.

Alikuwa tayari.

2 Tim. 4:6-8, "*Kwa maana mimi sasa namiminwa, na wakatika wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile wala si mimi tu bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*"

Je utakuwa tayari kufa leo? Kufanya hivyo unapaswa kuishi kwa Yesu.

Rum. 12:1, "*Basi ndugu zangu nawasii kwa huruma zake Mungu itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*"

Yesu anatuonya tuwe tayari katika kurudi kwake. Mathayo 24:42-44, "*Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi atakayo kuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakayokuja angalikesha wala asingeliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.*"

Mfano: Tatizo walilopata wanawali wapumbavu. Mat. 25:1-13, "*Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi waliotwaa taa zao wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia walala usingizi. Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya bwana arusi tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao. Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, tupeni mafuta yenu kidogo maana taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye busara wakajibu wakisema, sivyo hayatatutosha sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao mkajinunulie. Na hao walipokuwa wakienda kununua bwana arusi akaja, nao walio kuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa. Alafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema Bwana, Bwana utufungulie. Akajibu akasema, Amin nawaambia siwajui ninyi. Basi kesheni kwa sababu hamjui siku wala saa.*"

Lazima tukusudie na kupanga kwa ajili ya kuja Kwake.

## Hitimisho

Tumaini letu pekee la umilele ni kuwa tayari. Wale ambao hawako tayari watapotea. "Je uko tayari kwa siku hiyo ijayo?"

- Imani. Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." Nilipokuwa katika elimu ya juu (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na yangu, akaniambia kwamba haamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kuwa kuishi maisha ya Ukristo ni vizuri, lakini hakuwa na uhakika kama anaamini kwamba kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba anahudhuria kanisani na kuishi maisha mema Mungu atamruhusu kwenda mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "Haiendi hivyo. Unapaswa kumwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.*"

- Toba. Mdo. 2:38, "*Petro akwaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina ya Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi*

*mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kuna mwizi ndani ya nyumba yangu! Hivyo unachukua simu ya mkononi na kuwaambia polisi kuwa kuna mwizi ndani ya nyumba yako, na unawapa anwani yako. Ghafla, unasikia polisi wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, Samahani; Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadili maisha yake. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko ya tendo. Hivi ndio tunatakiwa kufanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- Kukiri. Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba andiko hilo hapo juu linasema kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "KATIKA" haki, uzima au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; siyo kwamba tayari mtu ameshapata.

- Ubatizo. Ni katika ubatizo ndio haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kutimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia. Kubali hivi sasa kwakua ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, na sio kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*…kwa ajili la*

*ondoleo la dhambi.*" Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka, asiye amini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16).

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale lazima utufie. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katikia upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neon hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katikia damu ya Kristo ndani ya maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kwa kuunyunyizia udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujafanyika jamii ya kundi la Mungu, kwa nini usizingatie leo?